# Dk. Mpango aitaka jamii kukemea unyanyasaji wa kijinsia nchini ..Uk.3

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.36 Tanzania Bora JUMANNE Machi 04, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




# Royal Tour ya Dk. Samia yavunja rekodi ongezeko la wanyama pori nchini

HABARI UK.2

>> Juhudi zake kutangaza utalii kwa vitendo ndani na nje ya nchi kupitia Programu ya Tanzania the Royal Tour imesaidia kuongeza hamasa kwa watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea hifadhi za utalii na Wanyamapori hapa nchini

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akishuhudia mashine ya mkono ya kutengeneza mkaa mbadala iliyobuniwa na Shirika la REDESO wakati akikagua mabanda katika Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Kanda ya Magharibi ikiwa ni shamrashamra kuelekea Siku ya Wanawake Duniani linalofanyika katika Ukumbi wa NSSF mkoani Kigoma jana tarehe 03 Machi 2025.*




# Ni marufuku kuswali Tarawehe Goma, DRC

NA MWANDISHI WETU

BARAZA kuu la Waislamu katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Limetoa Taarifa ya kusitishwa kwa Swala ya Taraweh Misikitini katika Miji ya mashariki nchini humo Goma,Bukavu, Uvira, Baraka na miji mingineyo

Inaendelea Uk. 2



# Msaada wa kisheria wa Dk. Samia wazidi kuwakomboa wanyonge

HABARI UK.2

# ROYAL TOUR YA DK SAMIA YAVUNJA REKODI ONGEZEKO LA WANYAMA PORI NCHINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana amesema ongezeko la idadi ya Wanyamapori katika hifadhi za Wanyama hapa nchini imetokana na juhudi za serikali kushirikisha wadau wa uhifadhi wa Wanyamapori na wananchi kwa ujumla hali iliyopelekea kukua kwa utalii na uchumi katika Taifa.

Ameyasema hayo jana jijini Dodoma katika maadhimisho ya 11 ya Siku ya Wanyamapori Duniani ambapo amesisitiza Tanzania inaongoza Duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wanyama aina ya Simba, Chui, Nyati na ni ya tatu kwa idadi wa Tembo Duniani huku akifafanua kuwa mafanikio hayo ni kutokana na kuitangaza vyema sera ya Utalii ndani na nje ya nchi na kuboresha jeshi la uhifadhi.

ìWanyamapori ni rasilimali muhimu katika uchumi wa nchi yetu kupitia utalii ambao unachangia zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni, asilimia 17.1 ya Pato la Taifa na ajira takribani milioni 1.6 zilizo rasmi na zisizo rasmi, hadi Mwaka 2024, Sekta ya Utalii imevunja rekodi kwa kufikia jumla ya watalii 5,360,247 na watalii wa Kimataifa imefikia 2,141,895 huku watalii wa ndani wakiwa 3,218,352. Kutokana na mapato ya utalii imefikia Dola za Marekani Bilioni 3.9î amesema Waziri Chana

Aidha, ameweka bayana kuwa juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii kwa vitendo ndani na nje ya nchi kupitia Programu ya Tanzania the Royal Tour na Amazing Tanzania imesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza hamasa kwa watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea hifadhi za utalii na Wanyamapori hapa nchini.

Katika hatua nyingine, Waziri Dk. Chana amesema Serikali kupitia Wizara Hiyo imeendelea kushirikiana na wadau wa uhifadhi kuchukua jitihada za makusudi ikiwemo kulinda na kuendeleza uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, kudhibiti ujangili wa nyara na kitoweo na uhifadhi endelevu wa mapito ya wanyamapori ili kuimarisha mifumo ikolojia ya uhifadhi sambamba na ushirikishwaji wa jamii kupitia maeneo ya Jumiya za Hifadhi za Wanyamapori.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayeshughulikia Maliasili, CP. Benedict Wakulyamba amesema Wizara itaendelea na mikakati ya kutunza na kuhifadhi Wanyamapori kwa kuweka mazingira wezeshi na kutangaza sera ya Utalii nje ya nchi kwa kukaribisha wawekezaji, kuboresha maeneo ya hifadhi, kuboresha maisha kwa watumishi na wahifadhi na vitendea kazi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Alexander Lobora amesema lengo la siku hiyo ni kuhamasisha Jamii juu ya Uhifadhi wa Wanyamapori pamoja na mimea iliyohatarini kutoweka, kupunguza uharibifu wa mazingira na kupinga ujangili.

“Siku hii adhimu inatoa fursa ya kutoa na kuonesha mchango kwa wahifadhi wa Wanyamapori na Wantama katika maisha ya bai anoai na hatua za kulinda Wanyamapori kwa manufaa ya Taifa kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho” amesema Dk. Lobora.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni “Wanyamapori na Uwekezaji Kifedha, Wekaza kwa watu na Dunia” inalenga kuhimiza mfumo na mikakati endelevu ya kusimamia na kutumia rasilimali fedha katika hifadhi wa rasilimali za Wanyamapori na nyara zake.



# NI MARUFUKU KUSWALI TARAWEHE GOMA, DRC

NA MWANDISHI WETU

BARAZA kuu la Waislamu katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Limetoa Taarifa ya kusitishwa kwa Swala ya Taraweh Misikitini katika Miji ya mashariki nchini humo Goma,Bukavu, Uvira, Baraka na miji mingineyo kwa sababu ya hali ya usalama hairuhusu kutoka nje nyakati za usiku

Baraza hilo limewataka waislamu wote maeneo hayo kuchanganya swala ya magharib na Swala ya Isha na kurejea majumbani kabla ya Giza kuingia.

Hatua hiyo imekuja kufuatia mashambulizi ya M23 ma majeshi ya Serikali ya DRC yalikuja kwa nguvu na kutishia ukanda huo, huku mateso, mauaji pamoja na vitisho vya milio ya silaha nzito zilizosambaa kila kona na kuzua hofu kwa wananchi wa nchi ya Kongo pamoja na ndugu na jamaa wa nchi mbalimbali waliokuwa na ndugu zao huko.

## Mara watakiwa kudumisha amani

NA MWANDISHI WETU

MKUU wa Mkoa wa Mara Kanali Evans Mtambi amesema serikali haitamvumilia mtu yoyote atakayetoa matamko yanayochochea uvunjifu wa amani na kuvuruga amani na utulivu kwa kisingizio cha siasa.

Badala yake amewataka wanasiasa kutoka vyama vyote wa Mkoa wa Mara, kufanya siasa zao kwa kuzingatia amani na utulivu kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025

Kiongozi huyo alitoa agizo hilo wakati anaongoza hafla ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara Machi Mosi, 2025 akiwatunuku askari waliofanya vizuri kwa mwaka 2024 katika viwanja vya FFU, Manispaa ya Musoma.

Mtambi aliwahakikishia wananchi kwamba Kamati ya Usalama ya Mkoa, imejiandaa kusimamia utulivu na haitamvumilia mtu yoyote anayefanya siasa za kupotosha umma.

Amewatahadharisha watendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama kuacha kujiingiza kwenye siasa isipokuwa kutumia haki yao ya msingi inayowaruhusu kupiga kura na kuchagua viongozi.

“Nalipongeza Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara kwa kazi nzuri wanayoifanya na askari wote waliopewa vyeti vya heshima na zawadi kwa kazi nzuri endeleeni kuiishi kauli mbiu yenu ya Nidhamu, Haki, Weledi na Uadilifu ili amani na usalama uliopo Mkoa wa Mara udumu”

Katika hatua nyingine amewataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuufanya Mkoa wa Mara kuwa sehemu salama kiuchumi na kuvutia wawekezaji na watalii.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara SACP Pius Lutumo, amesema utaratibu wa kuwatambua askari na wadau waliofanya vizuri lipo kwa mujibu wa taratibu za Jeshi hilo katika Utumishi wa Umma.

Amesema askari na wadau wamefanyakazi nzuri katika mwaka 2024 na kwamba wote waliohusika wamepewa vyeti na pesa taslimu shilingi 500,000 na kuwataka kuongeza bidii.

Kamanda amesema utoaji wa zawadi hizo ni tafsiri ya Inspekta Generali wa Polisi (IGP) kuhusiana na maelekezo yanayotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwapa askari mafunzo kazini, motisha na kuendelea kuwaondoa askari wanaotia doa jeshi hilo.

# DK. MPANGO AITAKA JAMII KUKEMEA UNYANYASAJI WA KIJINSIA NCHINI

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Watanzania kukemea vitendo vya ukatili ulioshamiri dhidi ya wanawake na watoto na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya wahusika.

Dkt. Philip Mpango alitoa wito huo wakati wa Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Kanda ya Magharibi lililofanyika katika Ukumbi wa NSSF mkoani Kigoma.

Ametaja baadhi ya vitendo hivyo kama mauaji, ubakaji, ulawiti, kupigwa, kunyanyaswa, kunyimwa haki za kumiliki ardhi na mali nyingine za familia, urithi, fursa za elimu, ukeketaji, adhabu kubwa zisizowiana na kosa alilotenda mtoto.

Makamu wa Rais amesema baadhi ya vitendo hivyo vinafanywa na wanafamilia au ndugu wa karibu na sehemu kubwa ya vitendo hivyo havitolewi taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Ameongeza kwamba wakati mwingine, baadhi ya mila na desturi katika jamii hutumika kuwakandamiza wanawake na watoto.

Aidha Makamu wa Rais ametoa rai kwa Kongamano hilo ambalo idadi kubwa ya washiriki wake ni wanawake na ambao ni walezi wa familia, kuelekeza nguvu pia katika kumlinda mtoto wa kiume ili kumhakikishia usalama wake. Amesema uwekezaji jitihada kidogo kwa mtoto wa kiume imepelekea mtoto wa kiume kujikuta katikati ya matatizo lukuki yakiwemo matumizi ya madawa ya kulevya, ushoga na aina nyingine za ukatili.

Makamu wa Rais ili kuendelea kuongeza mchango na ushiriki wa Wanawake katika utunzaji wa mazingira na kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia, hakuna budi kongamano hilo kujadili na kuibua mikakati madhubuti na yenye kutekelezeka ili kufikia malengo hayo.

Amesisitiza umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu na hamasa kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi ya kupikia. Amesema elimu kwa umma na hamasa ni muhimu katika utunzaji endelevu wa mazingira kwa kuwa tabiawatu ndiyo kisababishi kikuu cha uharibifu wa mazingira.

Makamu wa Rais ametoa rai kwa taasisi kama Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), TEMDO na nyingine kutafiti na kutengeneza teknolojia mbalimbali zinazotumia nishati safi na zenye gharama nafuu ili ziweze kusaidia uhamaji kwenda kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha ametoa wito kwa wafanyabiashara wakubwa na sekta binafsi kwa ujumla kujitolea kusaidia majiko na teknolojia rahisi kwa shule na vituo vinavyolea watoto na watu wenye mahitaji maalum.

Makamu wa Rais amesema Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 ñ 2034 ambao unalenga kuhakikisha 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Vilevile amesema Serikali imesaini makubaliano ya awali na wawekezaji kuhusu Ruzuku ya Sh. Bilioni 8.64 kwa ajili ya nishati safi ya kupikia, ambapo jumla ya majiko 452,455 yamepata ruzuku kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa wananchi kwa gharama nafuu.

Hali kadhalika Makamu wa Rais amewasihi wanawake kushiriki kikamilifu katika kutoa hamasa kuhusu jukumu muhimu la kujiandikisha kupiga kura, kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kushiriki kuchagua viongozi wanaowapenda. Amesema ni jukumu la kila mmoja kujenga na kudumisha umoja, amani, mshikamano na kuepuka vurugu katika mchakato wote wa uchaguzi.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Mwanaidi Ali Khamis amesema dhima ya kongamano hilo ni kuhimiza wanawake na jamii kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi. Amesema pia Kongamano limedhamiria kuhamasisha wanawake kukaa na familia pamoja na kupata muda mzuri zaidi ili kujenga malezi na makuzi kwa mustakbali wa familia bora.

Kongamano la wanawake kanda ya magharibi ni sehemu ya maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Wanawake Duniani ambayo kilele chake kitakuwa tarehe 8 Machi, 2025 Jijini Arusha. Kongamano hilo lina kaulimbiu isemayo ëMchango na ushi




# SERIKALI YATUMIA BIL 233.7 KUBORESHA VETA

NA MWANDISHI WETU

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufunzi Stadi (VETA), Anthony Kasore amesema serikali kwa mwaka 2021/2024 ilitenga kiasi cha Sh. 233.7 bilioni kwa ajili ya kufanya maboresho na ujenzi wa miundombinu ya VETA hapa nchini. Anaripoti Apaikunda Mosha. Dodoma Ö (endelea).

Hayo ameyasema jana, wakati anatoa taarifa kwa vyombo vya habari juu ya mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu na mafanikio ya mamlaka ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa mwaka 2021/24.

Kasore amesema, tangu uanzishwaji wake mwaka 1994 VETA ilipewa majukumu ya kuhakikisha kwamba inasimamia, kugharamia na kuratibu ufunzaji wa elimu ya ufundi stadi nchini, ili kuwe na mafundi mahiri wakutosha katika kutekeleza majukumu ya shughuli mbalimbali zinazohitaji rasilimali watu wenye ujuzi.

Akiainisha miradi mbalimbaliya maendeleo iliyofanywa na inayoendelea kufanywa amezungumzia kukamilika kwa ujenzi wa vyuo 33 katika wilaya 29 na mikoa minne, uliogharimu takribani bilioni 94.5, sambamba na hilo serikali imeendelea kuhakikisha ujenzi wa vyuo 64 unaendelea katika maeneo mbalimbali na tayari imetoa bilioni 103 kwa mradi huo.

Ameeleza pia, maboresho ambayo serikali imefanya katika vyuo vya VETA amesema kiasi takribani biloni 14.2 imetolewa kwa ajili ya maboresho katika vyuo ndani ya wilaya mbalimbali, na kwenye manunuzi ya vifaa vyenye ubora na vinavyokidhi mahitaji kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, takribani bilioni 22 zimetolewa ili waweze kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Aidha maboresho mengine ni kwenye uboreshaji wa mitaala 42, pamoja na kutengeneza mingine mipya 20 ambayo inajumuisha TEHAMA, michezo, umeme, magari, mitambo, kilimo, ukarimu, usafirishaji, biashara, mavazi, madini na urembo ili wawe na uwezo wa kujitengenezea kipato na kuliingizia taifa kipato.

Ameeleza pia katika vyuo vya kurekebisha tabia (magereza) jumla ya watu 214 katika vituo vya Ukonga, Arusha na Morogoro wameweza kufanyiwa tathmini ya ujuzi wao, na wamepatiwa vyeti ili waweze kuaminika nakufanya kazi ya kuridhisha.

Aidha katika program ya urasimishaji ujuzi ya Rais Samia amesema mpaka sasa wameshafanya urasimishaji wa watu 1600 na mpaka ifikapo juni 2026 wanatarajia kuwafikia zaidi ya wananchi 80,000 ili kuhakikisha uwa watu wanatambulika na wanapata zabuni mbalimbali.

# MSAADA WA KISHERIA WA DK. SAMIA WAZIDI KUWAKOMBOA WANYONGE




NA MWANDISHI WETU

MUITIKIO wa hali ya juu umejitokeza maeneo mbalimbali nchini wakati wa muendelezo wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia, ambapo Watanzania wengi wamefikiwa na kuupongeza mpango huo wanaoutaja kama ndiyo mkombozi wa wanyonge.

T ambapo wananchi wengi hasa wa kipato cha chini, wanafunzi, wajane na wahanga wengine wameonekana kurudishiwa matumaini ya kupata haki zao kutoka katika masuala mbalimbali.

Miungoni mwa mambo wanayotakiwa wahanga wanaokutana na wanasheria kwa ajili ya kupata msaada huo ni kutoa maelezo sahihi.

Hivi karibuni akiwa Jijini Arusha Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, aliwasisitiza wananchi kutoa maelezo sahihi kwa watoa huduma za msaada wa kisheria ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakabili.

Aliyataja maeneo yanayokumbwa na migogoro zaidi ni pamoja na ardhi, mirathi, ndoa na masuala mengine ya kisheria ambayo yanapata ufumbuzi.

Alitoa rai hiyo wakati alipotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mabanda mengine kuelekea wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo itafanyika Machi 8 mwaka huu mkoani Arusha.

Ukiacha maeneo mbalimbali ya nchi yaliyofikiwa na Kampeni hiyo, Wilayani Bagamoyo katika mkoa wa Pwani jumla ya wananchi elfu 14 kutoka kata nane zilizopo katika Halmashauri hiyo kutoka katika makundi mbali mbali waliokuwa wakikabiliwa na changamoto mbali mbali kama ndoa, mirathi, migogoro ya ardhi, pamoja na ukatili wa kijinsia wamefikiwa na kampeni hiyo ya msaada wa kisheria.

Wakiri George Molel ambaye ni mratibu wa huduma ya kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia katika Halmashauri ya Bagamoyo alisema kwamba lengo kubwa la msaada huo wa kisheria ni kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi ambayo itawasaidia kujua haki zao za msingi katika masuala mbali mbali.

Wakiri George amebainisha kwamba katika kampeni hiyo ya msaada wa kisheria Katika Halmashauri ya Bagamoyo imeweza kufanikiwa kupitika katika kata nane, zikiwemo Fukayose,Makurunge, Yombo, Kiromo,Kerege, Nianjema, Kisutu, pamoja na Kata ya Dunda ambapo wameweza kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu, wananchi wa kawaida, makanishani pamoja na makundi mbali mbali.

ìKampeni hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia imeanzishwa maalumu kwa lengo la kuweza kuwasaidia wananchi hasa wa hali ya chini kupata msaada wa kisheria kutoka kwa wataalamu mbali mbali kutoka Halmashauri pamoja na baadhi ya mawakiri kutoka Wizara ya Katiba na sheria na kwamba msaada huo unatolewa bila malipo yoyote lengo ikiwa ni kuwasaidia wananchi,îamesema Wakiri George.

Kwa upande wake Afisa maendeleo ya Jamii Kata ya Kerege Lilian Mkosyange amesema kuwepo kwa chanagmoto mbali mbali kwa wananchi ikiwemo suala la wakinababa kuwa na tabia ya kutelekeza familia zao na kupelekea mama na watoto kubaki peke yao bila msaada wowote.

Naye mmoja wakazi wa Wilaya ya Bagamoyo Samweli Ringo amempongeza kwa dhati Rais wa awamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuanzisha kampeni hiyo na kubainisha kwamba elimu ambayo wameipata itakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwani wameweza kujifunza mambo mbali mbali juu ya msaada wa kisheria.

Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inaendelea kufanyika katika Mkoa wa Pwani ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tayari imeshapita katika kata zipatazo nane na kutoa msaada wa kisheria katika masuala ya Ndoa, mirathi,migogoro ya ardhi, wosia,matunzo ya watoto,kesi za madai, unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na haki za binadamu na mambo mengine ya kimsingi yanayohitaji msaada huo.



# DK SAMIA ALIVYOONGEZA UWEZO UHIFADHI WA CHAKULA

NA MWANDISHI WETU

WAKALA wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula nchini (NFRA) umesema kuwa unajivunia mafanikio uliyoyapata katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza uwezo wa uhifadhi wa chakula cha akiba na ziada kuuza nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo Dkt Andrew Komba amesema katika kipindi cha miaka minne iliyopita, taasisi hiyo imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ya utendaji, ikiwemo kuongeza uwezo wa uhifadhi wa chakula cha akiba na kuuza takribani tani 600,000 za mazao katika masoko ya kimataifa .

ì Katika miaka ya nyuma, NFRA ilikuwa na uwezo wa kuuza kati ya tani 50,000-60,000 katika masoko ya kimataifa,î

ìLakini baada ya Serikali ya Rais Dkt Samia kutuwezesha, uhifadhi wa akiba ya chakula hapa nchini ili kukabiliana na upungufu utakapojitokeza umeongezeka,î

ìLakini pia tumeweza kuuza nje ya nchi chakula cha ziada na hii imesaidia kuinua maisha ya wakulima wetu na nchi kupata faida kutokana na mauzo hayo ya nafaka ya nje ya nchi,î amesema Dkt Komba.

Dkt Komba amesema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 NFRA ilikuwa na uwezo wa kuhifadhi shehena ya takribani tani 351,000, lakini hadi kufikia sasa, uwezo wa taasisi hiyo umeongezeka hadi kufikia kuhifadhi tarkiban tani 776,000.

Pia amesema kuwa kupitia mauzo ya nafaka, NFRA imekusanya takribani bilioni 540 ya mauzo ambapo fedha hizo zimekuwa zikitumika katika kupanua maeneo mbalimbali ya utendaji, ikiwemo ukarabati wa miundombinu na maghala.

ìMafanikio haya yanatokana na mizunguko ambayo Rais Samia amekuwa akiifanya katika nchi tofauti tofauti , akitumia nafasi hiyo kuinadi NFRA na kusaidia kupata masoko ya uhakika kwa nchi zenye uhitaji wa chakula,î amesema Dkt Komba.

Ameongeza kuwa kupitia Wizara ya Kilimo, Serikali imeiwezesha taasisi hiyo kuwa na maghala yenye uwezo wa kutunza jumla ya tani 48,000.

ìRais Samia akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Ruvuma mwaka jana alitukabidhi jumla ya maghala 28 yenye uwezo wa kuhifadhi takribani tani 28,000,î

ì Hivyo serikali kupitia wizara, imetusaidia ujenzi wa maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani takribani 76,000 za chakulaî Alisema Dkt Komba.

Katika kutanua wigo wa utendaji, NFRA Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita ilifanikiwa kuzindua maghala mengine mawili ambayo yalijengwa katika mikoa ya Katavi na Sumbawanga ili kuongeza uwezo wa maeneo ya uhifadhi wa akiba ya chakula.

ìIli kuhakikisha nchi inakuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha, Rais Dkt Samia aliiwekea NFRA malengo ya kuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030,î

ì Hivyo, Rais Samia , Waziri wa Wizara ya Kilimo Hussein Bashe pamoja na viongozi wengine wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha NFRA inafikia malengo haya î Alisema Dkt Komba

Amesema katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba mwaka 2024, NFRA imeweza kununua tani 479,000 kutoka kwa wakulima na manunuzi haya hayajawahi kufanyika katika taasisi hiyo katika miaka ya nyuma.

NFRA ina jumla ya tani 776,000 katika maghala yake ambapo kati ya hizo tani 400,000 zitauzwa katika masoko ya ndani na nje na tani 300,000 zitabakishwa katika maghala kwa ajili ya kulinda usalama wa chakula nchini.

Endapo uzalishaji wa chakula kutoka kwa wakulima utapungua, Dkt Komba amesema NFRA itakuwa na uwezo wa kuilisha nchi kwa mwaka mzima.

ìkwa sasa NFRA inashehena yakutosha ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya kuuza mazao katika masoko ya ndani na nje pia itaendelea kuwa na shehena ambayo itasaidia kulisha nchi endapo majanga ya njaa au maafa yatatokeaî.Alisema Dkt Komba

# TANZANIA KUNUFAIKA NA UCHIMBAJI WA MADINI AINA ADIMU

NA MWANDISHI WETU

IMETHIBITISHWA kwamba Madini ya Niobium ni moja ya madini adimu na muhimu katika sekta ya teknolojia , ujenzi na matumizi ya viwandani hasa katika utengenezaji wa vifaa vya superalloys vinavyotumika katika anga za juu, magari ya kisasa pamoja vifaa vinavyostahimili joto kali. . Vilevile kutengeza sumaku kwenye mota za magari ya umeme , betri za magari ya mseto na umeme;na vitu vingine mbalimbali vya umeme.

Sambamba na matumizi katika nyanja za sayansi na teknolojia pia madini ya Niobium hutumika katika mitambo ya uchorongaji katika tafiti na uchakataji wa mafuta na gesi.

Naibu Waziri wa madini Dkt. Steven Kiruswa alieleza kuwa Tanzania inatarajia kuanza uzalishaji wa madini ya Niobium kupitia mradi wa Mamba Minerals Corporation Limited (MML), kampuni ya ubia katika ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye Hisa asilimia 16% na kampuni ya Peak Resources Ngualla Company (PRNG) ya nchini Australia yenye asiliamia 84%.

MML ni kampuni inayomilika leseni kubwa ya uchimbaji (Special Mining licence- SML) wa Madini Mkakati (Critical Minerals) yenye jina la Rare Earth Elements. Mradi upo kijiji cha Ngwala, Mkoani Songwe, takribani km 1000 kutokea Dar es Salaam na km 150 kutokea Mbeya Mjini; Uhai wa mgodi unakadiriwa kuwa miaka 24.

Pamoja na mambo mengine , katika mahojiano na kituo cha televisheni cha CNBC Africa wakati wa mkutano wa Indaba Mining 2024 nchini Afrika Kusini , Dkt. Kiruswa alielezea kuhusu uwepo wa madini muhimu yaliyopo Tanzania yakiwemo madini ya Niobium pamoja na mikakati ya uwekezaji katika maeneo yenye rasilimali hizo.

Madini ya Niobium yatakayochimbwa yataongezewa thamani nchini kwa kuchanganywa na madini ya chuma ili kuzalisha *ferroniobium*, bidhaa inayohitajika katika masoko ya nchi za Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini.

Tanzania itafaidika kwa namna mbalimbali katika uchimbaji wa madini ya Niobium ikiwemo, Kuongeza Mapato ya Serikali, kuimarisha Sekta ya Viwanda na Teknolojia, Kuhamasisha Uwekezaji wa Ndani na Nje.

Nchi zinazoongoza kwa uchimbaji wa Niobium Afrika ni pamoja na Msumbiji ambayo ina mradi wa Mozambique Niobium Project, Rwanda kupitia uzalishaji wa madini ya tantalite na cobalt ambayo uambatana na Niobium, nchi nyingine ni Afrika Kusini.

# DHAMIRA YA SERIKALI KUANZISHA MIFUKO NI KUWANUFAISHA WANANCHI



NA MWANDISHI WETU

SERIKALI ilianzisha mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya kuwanufaisha wanachama wanaojiunga nayo kwa manufaa ya baadaye hasa baada ya kufikia umri wa kukoma kufanya kazi. Mifuko hiyo ilikuwa ikitoa mafao mbalimbali kwa wanachama , hivyo kuwawezesha kuishi kwa amani na furaha baada ya kustaafu.

Baada ya kuona kuna mifuko mingi ambayo ilikuwa ikiwahudumia wanachama na baadhi kutofanya kazi kwa ufanisi, serikali iliamua kuiunganisha na kubaki na mifuko mwili tu ambayo ni wa pensheni kwa watumishi wa umma (PSSSF) na ule wa wafanyakazi wa sekta binafsi (NSSF).

> **Kwa ujumla, skimu hiyo itakuwa mkombozi kwa wengi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq, ambaye pia alipongeza NSSF kwa kuboresha.**

Hata kabla ya kuunganishwa na kubaki na hiyo miwili, mifuko hiyo ilikuwa ikivutia makundi mbalimbali wakiwamo wale waliojiajiri ili kujiunga kwa ajili ya kuwasaidia baadaye. Wanachama wa mifuko hiyo walikuwa wanapata mafao mbalimbali kama kiinua mgongo, mazishi, kujitoa, afya na elimu.

Kwa kufanya hivyo, watu mbalimbali kutoka kwenye makundi tofauti walikuwa wakijiunga kwa kulipa kidogo kidogo kila mwezi na hatimaye miongoni mwao walinufaika.

Kutokana na kuwapo kwa mifuko miwili baada ya kuunganishwa, NSSF imeibuka na skimu mpya iliyoboreshwa kwa sekta isiyo rasmi (NISS) kwa lengo la kuwafikia Watanzania wengi zaidi waliojiajiri ili kunufaika na mafao yanayotolewa na mfuko huo.

Akifungua mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, mapema wiki hii jijini Dodoma, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, alisema skimu hiyo imetengenezwa vizuri na ina faida kubwa kwa jamii. Kwa mujibu wa Waziri Kikwete, skimu hiyo inatoa kinga dhidi ya majanga kama uzee, ulemavu na ugonjwa kwa walengwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema skimu hiyo imeanzishwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi waliojiajiri katika shughuli za kiuchumi huku akiwataja wanufaika na walengwa kuwa ni wakulima, wavuvi, wafugaji, wachimbaji wadogo wa madini, mama na baba lishe, waendesha bodaboda na wajasiriamali wengine wote.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu huyo, ili kunufaika, mwanachama anapaswa kuchangia Sh. 30,000 na atanufaika na fao la matibabu au Sh. 52,200 ambazo atanufaika na matibabu yeye na familia yake. Pia ni rahisi kuchangia kwa kuwa mwanachama anaweza kuchangia kidogo kidogo kwa siku, wiki au mwezi kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo atayopewa.

Kwa ujumla, skimu hiyo itakuwa mkombozi kwa wengi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq, ambaye pia alipongeza NSSF kwa kuboresha skimu hiyo ambayo itawanufaisha wananchi waliojiajiri kwa kunufaika na mafao mbalimbali yanayotolewa na mfuko.

Ni vyema sasa makundi yaliyotajwa kuwa ndiyo walengwa yanapaswa kuchangamkia fursa hiyo ili kunufaika na mafao mbalimbali yakiwamo matibabu kwa siku zijazo. Kama ilivyoelezwa namna ya kujiunga, ni jambo rahisi kwa sababu katika maisha ya kawaida, na ya kila siku, hakuna mtu mwenye dhamira ya dhati ya mafanikio ya baadaye kuwekeza sasa.

Mfumo wa kujiunga na skimu hiyo ni wa udundulizaji na kwa kadri hali ilivyo kwa makundi hayo, kama kuna dhamira ya dhati kutoka moyoni, wengi wana uwezo wa kujiunga kwa manufaa yao ya baadaye. Jambo la kujiuliza ni nani ambaye anaweza kushindwa kundunduliza kila siku, wiki au mwezi ili kunufaika na mfuko huo?

Suala la matibabu, mathalani, limekuwa likiwasumbua wengi hasa wale wasiokuwa na bima ya afya, hivyo ni fursa kwa makundi hayo kujiunga na skimu ya NSSF kwa manufaa yao na familia zao kwa siku zijazo.

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakukuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


**BODI YA UHARIRI**

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

**MAWASILIANO**

JAMVI MEDIA GROUP




*Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa akizungumza jambo na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi, walipokutana Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hosea Kutako, Windhoek, nchini Namibia, baada ya mazishi ya Rais wa Kwanza wa Namibia na Baba wa Taifa hilo, Dk. Sam Shafiishuna Nujoma, mwishoni mwa wiki.*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# SERIKALI YATOA MSUKUMO KUBORESHA ZAO LA KAHAWA



NA MWANDISHI WETU

KAHAWA ni kinywaji maarufu duniani na ni moja ya bidhaa muhimu katika soko la dunia ikishika nafasi ya nne baada ya mafuta, dhahabu na gesi asilia.

Uzalishaji wa kahawa nchini umechangia upatikanaji wa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kuanzia kwa wakulima, viwandani na hata kwenye biashara za kimataifa.

Mauzo ya kahawa ya Tanzania nje ya nchi yameongezeka kufika zaidi ya Dola za Marekani milioni 230 kutoka Dola za Marekani milioni 140, sambamba na kuongezeka uzalishaji wa kahawa kutoka tani milioni 34 hadi kufikia tani milioni 85 mwaka jana.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe anasema kuwa kahawa ni miongoni mwa mazao ya biashara ambayo kumekuwa na mikakati mingi katika kuhakikisha uzalishaji unaongezeka na kuwa na viwanda vya kuongeza thamani ili kupunguza

mauzo ya zao hilo nje ya nchi.

ìTumeweka malengo ya miaka 10 ijayo, ni kuhakikisha asilimia 50 ya kahawa inayozalishwa Afrika inaongezewa thamani ili kupunguza mauzo ya kahawa ghafi nje ya nchi,î anasema.

Bashe anasema kuwa suala la kuongeza thamani kahawa kwa kutumia miundombinu iliyopo ni ajenda ya kudumu.

ìLicha ya kuongezeka kwa uzalishaji wa kahawa kutoka tani milioni 34 hadi kufikia tani milioni 85 bado kuna changamoto ya uuzaji kahawa ghafi kutokana na ukosefu wa viwanda hali ambayo imekuwa ikichangia kupungua kwa mapato,îanasema Waziri Bashe.

Anabainisha kuwa thamani ya biashara ya kahawa duniani ni dola bilioni 500 na Afrika ina uzalishaji wa asilimia 50 lakini inapata dola bilioni 2.5 tu ya mapato yote.

Pia, anasema pamoja na kuzalisha kiasi kikubwa na kupokea kiasi kidogo bado uagizaji wa kahawa iliyosindikwa kutoka nje ni mkubwa.

ìLicha ya kuwa wazalishaji wakubwa wa kahawa, tunauza bilioni 2.5 lakini tunaagiza kahawa zaidi ya Sh bilioni sita,î anasema.

Anasema kuwa miongoni mwa mikakati ambayo nchi imeweka ili kuongeza uzalishaji wa kahawa ni pamoja na kusambaza miche milioni 20 ya kahawa bure kwa wakulima.

Anasema kuwa usambazaji wa miche ya kahawa utachangia kuongeza uzalishaji. Pia, anabainisha kuwa ajira za kahawa zinatengenezwa shambani ikiwemo kukaanga, kubangua, kusaga, kufungasha na kuuza lakini kwenye mnyororo wa thamani kuna hatua mbili tu nyingine zote zinapelekwa nje ya nchi.

Tanzania imekuwa ikizalisha kahawa aina ya Arabika na Robusta. Maeneo ya kilimo cha Arabika ni Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Iringa, Mbeya, Kigoma, Manyara, Mwanza, Katavi, Mara, Njombe, Songwe, Rukwa, Geita na Ruvuma.

Pia, kahawa aina ya Robusta inalimwa katika mikoa ya Kagera na Morogoro. Ni katika jitihada hizo za kuongeza uzalishaji na thamani ya zao la kahawa, Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tatu wa Nchi Zinazozalisha Kahawa Afrika (G25 African Coffee Summit).

Akizungumzia mkutano huo Waziri Bashe anasema unatarajiwa kufanyika Februari 21 mwaka huu jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Anasema mkutano huo unaoandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Kahawa la Afrika (IACO) utahudhuriwa na Wakuu wa Nchi zinazolima Kahawa Barani Afrika, Mawaziri wa Kilimo, Sekta Binafsi na Viongozi wa Taasisi za Kahawa katika nchi zinazolima zao hilo Afrika. Wengine ni wakulima na wadau katika mnyororo wa thamani wa Kahawa.

Anasema mkutano huo utaongozwa na kaulimbiu ya Mkutano huo ni ëKufungua fursa za ajira kwa vijana kupitia

uboreshaji wa Sekta ya Kahawa Afrika.î

Bashe anasema mkutano huo utatoa mwongozo wa jinsi ya kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU) na Mashirika yake, Benki za Maendeleo za Afrika na taasisi nyingine za fedha ili kuunda programu zinazochochea ujasiriamali na ajira kwa vijana kupitia Sekta ya Kahawa.

Anasema kuwa kwa upande wa Tanzania, utekelezaji huo umeanza kupitia Wizara ya Kilimo ambayo imezindua programu ya ujasiriamali kwa vijana uitwao Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT), moja ya mipango ikiwa ni kuanzisha

ëmaduka ya kahawa yanayotembeaí ili kuchochea na kuongeza idadi ya watumiaji nchini.

Anaongeza kuwa migahawa hiyo, itawawezesha vijana wajasiriamali kujiajiri kwa kuuza kahawa katika maeneo mbalimbali ikiwemo barabarani kwa wapita njia, kwenye matukio ya umma na kijamii, vyuo vikuu na hospitali.

Pia, anasema serikali kupitia wizara ina mpango wa kuanzisha Vituo vya Umahiri vya Kahawa kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu ili kuelimisha vijana kuhusu mnyororo mzima wa thamani wa kahawa kutoka uzalishaji hadi unywaji.

Anasema kuwa mpango wa kuanzisha mkutano wa nchi wazalishaji wa kahawa Afrika ni matokeo ya azimio

lililopitishwa wakati wa Mkutano wa 61 wa Mwaka wa IACO uliofanyika Kigali, Rwanda, Novemba 2021, la kuandaa mkutano wa ngazi ya juu wa nchi 25 zinazozalisha zao hilo Afrika ili kutathmini mapungufu na changamoto zinazosababisha kudumaa kwa wa Sekta ya Kahawa.

Baada ya kupitishwa kwa azimio hilo, mkutano wa kwanza ulifanyika Kenya Mei 2022, na ulipitisha ëTamko la Nairobií, lililoazimia kuweka mkakati wa kuingiza kahawa kama bidhaa muhimu ya kimkakati katika Umoja wa

Aidha, Bashe anasema Mkutano wa pili wa nchi wazalishaji wa kahawa Afrika uliofanyika Kampala, Uganda, Agosti 2023, ulipitisha ëTamko la Kampalaí, lililokusudia kuwaomba Wakuu wa Nchi 25 zinazozalisha kahawa barani Afrika kuunga mkono kuidhinishwa na kujumuishwa kwa zao hilo kama bidhaa muhimu ya mkakati katika Ajenda ya 2063 ya AU na kuifanya IACO kuwa shirika maalumu la Umoja wa Afrika.

Katika kikao cha 37 cha kawaida cha Baraza Kuu la Umoja wa Afrika kilichofanyika Februari 2024, Addis Ababa, Ethiopia wakuu wa nchi na Serikali walipitisha kwa kauli moja kuingiza zao hilo kama bidhaa muhimu ya mkakati katika Agenda ya 2063 ya AU na kuifanya IACO kuwa shirika maalumu la Umoja wa Afrika.

Moja ya hatua zilizochukuliwa katika kutatua changamoto za biashara ya kahawa baina ya nchi za Afrika ni kuanzishwa kwa Mkataba wa Biashara Huria Afrika (AfCFTA) wa 2018 kwa lengo la kuondoa vikwazo vya biashara katika ya nchi za Africa na hivyo utekelezaji kamili wa mkataba huo utaimarisha biashara ya kahawa bila vizuizi baina ya nchi za Africa.

Mkutano huo wa tatu utajadili maeneo muhimu katika mnyororo wa thamani wa kahawa kwa ajili ya kufungua fursa za biashara na ajira kwa vijana.




Matukio mbalimbali ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Philip Mpango akishiriki katika Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Kanda ya Magharibi ikiwa ni shamrashamra kuelekea Siku ya Wanawake Duniani linalofanyika katika Ukumbi wa NSSF mkoani Kigoma, jana.







Matukio mbalimbali ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Philip Mpango akishiriki katika Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Kanda ya Magharibi ikiwa ni shamrashamra kuelekea Siku ya Wanawake Duniani linalofanyika katika Ukumbi wa NSSF mkoani Kigoma, jana.

# SERIKALI YATAKA WANAUME WAEWE WALINZI DHIDI YA WANAWAKE



NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, Wazee, na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Riziki Pembe Juma, amewataka wanaume kuwa mstari wa mbele katika kuwalinda wanawake na watoto badala ya kuwa chanzo cha vikwazo.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake na Wanawake Wenye Ulemavu yaliyofanyika Mkoani Shinyanga leo, Machi 1, 2025, Mhe. Riziki ameweka wazi kuwa jamii inapaswa kushirikiana kwa pamoja ili kuimarisha haki, usawa, na uwekezaji, akisisitiza kuwa wanaume wanahitaji kuchukua jukumu kubwa la kuwalinda wanawake, watoto, na watu wenye ulemavu.

Maadhimisho hayo yameandaliwa na Shujaa Wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali yakiongozwa na kauli mbiuìWanawake na Wasichana 2025, Tuimarishe Haki, Usawa na Uwekezajiî.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, Wazee, na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Riziki Pembe Juma

ìTuendelee kupinga ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Wenye silaha za kufanyia ukatili ni wanaume, wenye silaha za ubakaji na ulawiti ni wanaume, naomba akina baba silaha zihifadhini vizuri, zitumike vizuri, pahala sahihi kwa watu sahihi, zisitumike kwa watoto wetuÓ zisionekane hovyoî,amesema Mhe. Riziki.

> **Amesema changamoto zingine zinazowakabili wanawake wenye ulemavu, kama vile ukatili wa kijinsia, unyanyapaa, na ubaguzi katika jamii.**

Aidha, Mhe. Riziki ametoa wito kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi ujao wa 2025, akisema kwamba wanawake wanapaswa kujiandaa kushiriki kwa wingi ili kuungana na viongozi wanaume katika kuboresha maendeleo ya taifa.

Amewashauri wanaume kuwa mstari wa mbele kumuunga mkono mgombea mwanamke ili kuongeza uwakilishi wa wanawake katika uongozi, akisemaìWanawake wanapokuwa katika uongozi, huongeza mchango wa uchumi wa familia na jamii nzima.î

Mhe. Riziki pia amewapongeza wanawake wenye ulemavu kwa bidii na juhudi zao katika kuchangia maendeleo ya jamii, akisisitiza umuhimu wa ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali kuhakikisha kundi hilo linapata nafasi sawa katika sekta zote.

ìSiku ya Wanawake Duniani ni fursa ya kutambua mchango wa wanawake wote, wakiwemo wenye ulemavu, katika maendeleo ya taifa. Ni jukumu letu kuhakikisha wanapata haki zao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi,îamesema Mhe. Riziki.

Amesema wanawake wenye ulemavu wanastahili pongezi kwa mchango wao katika jamii licha ya changamoto wanazokutana nazo, na kusema,ìSiku ya Wanawake Duniani ni alama muhimu ya kutambua mchango wa wanawake wote, bila kujali hali zao. Tunapaswa kuhakikisha kuwa wanawake wenye ulemavu wanapata nafasi sawa katika elimu, ajira, na uongozi, ili wawe sehemu ya maendeleo ya nchi.î

Aidha, ameongeza kuwa serikali inaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha huduma za jamii kwa wanawake wote, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa elimu, huduma za afya, na maji safi, ili kuhakikisha wanapata mazingira bora ya maisha.

Akisoma risala, Katibu wa Idara ya Wenye Ulemavu SMAUJATA Taifa, Imani Axwesso, amebainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake wenye ulemavu, ikiwemo ukosefu wa ajira, mitaji ya biashara, mikopo, na nafasi za uongozi.

ìJamii inapaswa kuhakikisha kuwa wanawake wenye ulemavu wanashirikishwa kikamilifu katika nafasi za kimaendeleo ili waweze kujitegemea na kushiriki katika maamuzi ya uongozi,îamesema Axwesso.

Amesema changamoto zingine zinazowakabili wanawake wenye ulemavu, kama vile ukatili wa kijinsia, unyanyapaa, na ubaguzi katika jamii.

Aidha, amehimiza serikali na wadau wa maendeleo kuweka mikakati madhubuti ya kuwawezesha kiuchumi, na kuhakikisha wanapata huduma bora za elimu na afya.

Kwa upande mwingine, amehamasisha umuhimu wa malezi bora kwa watoto, hasa akijikita katika kutoa ushauri kwa wazazi na walezi kuwaepusha watoto na mazingira hatarishi, kama vile kuwalaza na wageni, ili kuepuka ukatili wa kijinsia.

ìKila kundi linapaswa kulindwa. Tuache ukatili wa kijinsia. Tunawapongeza SMAUJATA kwa jitihada zao za kupambana na ukatili wa kijinsia,îameongeza Mhe. Riziki.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Mhe. Patrobas Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na watu wenye ulemavu amekiri juhudi za serikali katika kuboresha hali ya maisha kwa watu wenye ulemavu, hasa wanawake na watoto, kupitia mikopo na ajira.

Vilevile, amesema kuwa haki za watu wenye ulemavu zitazidi kuimarishwa na serikali itaendelea kutekeleza sheria na taratibu zinazolinda haki zao.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Anamringi Macha, amesema kuwa serikali na wadau wameendelea kushirikiana katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia, na ameelezea matumaini kuwa vita dhidi ya ukatili wa kijinsia itashinda, akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kupigania haki za wanawake na watoto.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Dkt. Christina Mzava, ameelezea mfano bora wa Rais Samia Suluhu, ambaye anapigania haki za wanawake na wanawake wenye ulemavu.

ìMwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, wanawake na watu wenye ulemavu, tusikubali kubaki nyuma. Tuchukue fomu na tushiriki katika nafasi za uongozi ili kuwa na sauti katika ngazi za maamuzi,îamesema.

Mwenyekiti wa SMAUJATA Taifa, Sospeter Mosewe Bulugu, amewakumbusha wanaume kuacha kunyanyasa wanawake na kuhakikisha wanawake wanapata usalama, huku akisisitiza umuhimu wa kushirikisha wanawake wenye ulemavu katika masuala ya uongozi.

Amesema kuwa SMAUJATA ni jumuiya ya kijamii inayolenga kuchochea mabadiliko chanya na kuleta maendeleo endelevu kijamii na kiuchumi na ilianzishwa ili kuchochea shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii, huku akieleza kuwa ilizinduliwa rasmi na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima, mnamo Juni 16, 2022.

ìDira ya SMAUJATA ni kuwa na taifa lenye kizazi huru chenye haki na usawa, kitakachoweza kujitegemea na kuzitambua fursa, na kutumia ujuzi, maarifa, na vipaji katika kujenga jamii yenye maendeleo endelevu,îamesema Bulugu.

# MAPATO BANDARI YA TANGA YANAVYOZIDI KUPAA



NA MWANDISHI MAALUM

MKUU wa Mkoa wa Tanga Mhe. Batilda Buriani, amewaambia wakazi wa Tanga kuwa ndani ya Miezi mitano tangu kutanuliwa na kuboreshwa kwa Bandari ya Tanga kulikofanywa na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, Jumla ya takribani Shilingi bilioni 100 zimepatikana kama faida inayotokana na bandari hiyo na hivyo kusisimua na kukuza uchumi wa mkoa huo na kanda nzima ya Kaskazini mwa Tanzania.

Mkuu wa Mkoa huo Mhe.Batilda ameeleza hayo mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa Mkutano wa hadhara unaofanyika kwenye viwanja vya Mkwakwani Jijini Tanga, akimshukuru Rais Samia kwa kuikumbuka Tanga na kupeleka miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani humo ya takribani Trilioni 3.1

Wakati wa siku yake ya sita ya ziara Mkoani humo, Mhe. Batilda amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan pia kwa kurejesha ajenda ya viwanda Mkoani Tanga, akisema Ujenzi wa viwanda kilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wakazi wa Tanga kwani kutasaidia pia kuongeza na kuzalisha fursa mpya za ajira kwa Vijana wa Tanga.

Utendaji wa Bandari ya Tanga, umeimarika kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni kutokana na uwekezaji mkubwa wa serikali ambapo Bandari hiyo ilijengwa kwa mara ya kwanza mwaka 1914, ili kukidhi mahitaji ya kibiashara na kilimo kaskazini mwa Tanzania.

Ni bandari iliyopata uwekezaji mkubwa wa umma katika kipindi cha miaka minne iliyopita na kuiweka katika ramani ya kimataifa, kama kituo muhimu kwa meli kubwa.

Maboresho katika Bandari ya Tanga yalifanyika kwa awamu mbili ikiwa ni pamoja na kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13 na kupanua njia ya meli kugeuza. Mradi pia ulijumuisha ununuzi wa vifaa vipya vya kushughulikia mizigo na upanuzi wa gati mbili katika bandari hadi upana wa mita 450.

Maboresho hayo pia yameimarisha utendaji kazi wa Bandari ya Tanga, yakiwezesha bandari kupakua mizigo kutoka kwa meli kubwa ndani ya siku mbili, tofauti na siku tano au zaidi zilizokuwa zinahitajika awali.

Kwa mwingine hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini Mrisho Gambo amesema ndani ya miaka minne ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan Mkoa wa Arusha kwa ujumla hisusani jimbo lake wamekuwa wanufaika wakubwa wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Gambo ameyasema hayo leo Jumatano Februari 19, 2025 wakati akizungumza na na Wazee wa Wilaya ya Arusha huku akiwahimiza kumchagua kwa kishindo Rais Samia kwenye uchaguzi mkuu ujao, akisema mkutano mkuu wa CCM haukukosea kumpitisha kuwa mgombea pekee kwenye uchaguzi huo.

Gambo amekutana na wazee hao kama sehemu ya utaratibu wake wa kukutana na makundi mbalimbali ya kijamii katika kuwapatia elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ambako pia amegawa majiko ya gesi kwa wazee 182 waliohudhuria mkutano huo.

Akiitaja baadhi ya miradi hiyo, Gambo amesema kata ya Sombetini, Osunyai na Ungalimited ni miongoni mwa wanufaika wa miradi mikubwa ya barabara ikiwemo ya Mbauda Simanjiro, ambayo itajengwa kwa kiwango cha Lami kwa njia nne, suala ambalo litaondoa changamoto ya usafiri na usafirishaji hasa nyakati za mvua.

Ameizungumzia pia barabara ya Kilombero mpaka uwanja wa ndege wa Arusha Kisongo ambayo ujenzi wake ulikuwa ukisuasua tangu mwaka 2020, na Rais Samia alipoingia madarakani tayari usanifu umefanyika, fidia ya Sh. Bilioni 10 imeshaanza kulipwa kwa wananchi na tayari.

"Mchakato wa ujenzi wake umeanza katika jitihada za kuondoa msongamano wa magari kwenye Jiji hilo la Arusha sambamba na kuondoa usumbufu kwa wanaofika jijini hapo kwa kutumia uwanja wa ndege wa Arusha wakiwemo watalii," amesema Gambo.

Ameongeza kuwa Rais Samia ndani ya miaka minne ya uongozi wake amefanikisha kuupeleka mradi wa TACTICS jijini humo, mradi ambao utajenga kituo kikubwa cha kisasa cha mabasi Jijini Arusha.

Pia utasaidia kujengwa soko la Kilombero pamoja na soko la Morombo ambako kufikia mwezi Juni mwaka huu, mkandarasi atakuwa amepatikana na kuanza kazi mara moja.

# JUHUDI ZINAHITAJIKA ZAIDI KUOKOA MAISHA YA MAJERUHI GOMA

NA MWANDISHI WETU

GHASIA za hivi karibuni huko Goma, Kivu Kaskazini, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC, kuanzia mwishoni mwa mwezi Januari zimeongeza mahitaji ya huduma za afya. Ili kukabiliana na hali hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani (WHO) limechangia vifaa muhimu vya matibabu, ikiwa ni pamoja na mahema na vitanda, kwa vituo vya afya ili kusaidia katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa. Kupitia video iliyoandaliwa na WHO.

Video iliyorekodiwa kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu wa Februari 2025 hadi majuzi, inaanzia juu angani kuonesha madhari ya mji wa Goma, kisha inashuka chini mtaani ambako pilika za siku zinaendelea.

Na sasa video hiyo inatupeleka katika Hospitali ya Rufaa ya Goma. Dkt Jean Bruno ambaye ni Mkuu wa Ofisi ya WHO Kivu Kaskazini anaingia katika moja ya mahema yaliyoko hapa yakitumika kama wodi za muda za WHO na anaonekana akizungumza na wagonjwa wanaopata huduma hapa. Yuko katika hema la wanawake.

Dkt. Jean Bruno baada ya kuzungumza na wagonjwa, sasa ametoka ndani, anazungumza kwa matumaini akisema,

"Katika jiji la Goma kwa sasa. Utulivu unarejea polepole. Tunaweza pia kuona kuwa shughuli za kijamii na kiuchumi zimeanza kurejea taratibu."

Video hii inaonesha sasa mafundi chini ya usimamizi wa maafisa wa shirika la Msalaba Mwekundu na WHO wakisimika mahema mengine zaidi katika maegesho ya magari ya hospital hii ya rufaa ya Kivu Kaskazini. Vyuma na maturubai meupe vinatolewa katika makasha makubwa ya mbao, vinasimamishwa na kuunda mahema ambayo kila moja linatoa nafasi ya kuweka vitanda 20 vya wagonjwa, kumi kila upande.

Wahudumu wa afya katika hospitali ya Goma watoa msaada kwa waathiriwa wa mapigano katika siku za hivi majuzi.

Dkt Jean Bruno na Dkt Gaston Lubin wanajadiliana jambo. Dkt Gaston Lubin, ni Mganga Mkuu katika Hospitalini hapa anaeleza kwa nini kinachoendelea hapa ni muhimu,

"Kwa sababu kulikuwa na majeruhi wengi, ilihitajika kuongeza nafasi kwa kusimika mahema. Lakini mahema yaliyowekwa pia yana magodoro. Hili limewezesha kupokea wagonjwa wengi na kutoa huduma zinazofaa kulingana na aina za majeraha yaliyokuwepo."

Bada ya hapo Dkt Jean Bruno anaingia katika hema jingine, sasa ni la wanaume, anazungumza na mmoja wa wagonjwa anayeitwa Zulu Augustin.

Zulu Augustin analo la kusema, "Hapa hospitalini, tunaishi vizuri, tunasimamiwa vyema na kulindwa vizuri. Tunapewa kila kitu kwa ajili ya kula, dawa, na kila kitu kiko sawa."

Zulu Augustin ni majeruhi, ana majeraha kuanzia usoni hadi miguuni, anaeleza kilichosababisha majeraha kwenye mwili wake akisema, "Kulikuwa na vipande vya mabomu vilivyoingia na pia risasi. Tuliitoa risasi, lakini haikugonga mfupa. Ndio, kwa sasa hali ni nzuri."

Dkt Jean Bruno, kama nilivyoeleza awali yeye ni Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani Kivu Kaskazini bado yuko hapa anazungumza na wagonjwa na baada ya kutoka ndani anaeleza changamoto akisema,

"Ukweli ni kwamba hatuna rasilimali za kutosha, hasa rasilimali za kifedha, kutoa msaada wote unaohitajika. Kuna changamoto tunazoweza kuzingatia, kama vile kusaidia wagonjwa kwa ajili ya mwendelezo wa matibabu, lakini pia utambuzi, utafiti na urejeshaji wa wagonjwa, hasa wale wenye magonjwa ya kuambukiza, kama vile waliokuwa na surua, kipindupindu au mpox, ambao walijikuta katika jamii. Hivyo basi, utafutaji wa haya pia ni changamoto kwa sasa."

Umoja wa Mataifa kupitia mashirika yake na wadau wake wengine wameendelea kujitahidi kuhudumia jamii ya mashariki mwa DRC japo katika mazingira magumu kutokana na hali tete ya usalama inayotatiza pia usafiri kwa wafanyakazi na vifaa.



Inaendelea Uk. 13

# JUHUDI ZINAHITAJIKA ZAIDI KUOKOA MAISHA YA MAJERUHI GOMA

Inatoka Uk. 12

Tangu mapigano ya hivi karibuni katika ya jeshi la DRC na waasi wa M23 yalipopamba moto, yamechochea joto zaidi la changamoto za wananchi wa eneo hilo.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa AntÛnio Guterres, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa 58 wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, huko jijini Geneva, Uswisi, ameshutumu vikali wachochezi wa vita wanaodharau sheria za kimataifa, sheria za kibinadamu za kimataifa na Katiba ya Umoja wa Mataifa na akasisitiza matumizi ya diplomasia katika kutatua migogoro ulimwenguni.

Hivi karibuni Muungano wa waasi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Alliance Fleuve Congo (AFC), unaojumuisha waasi wa M23, umetangaza kuwa tayari kushiriki mazungumzo na serikali ili kusitisha mara moja mapigano




mashariki mwa nchi, msemaji wa kundi hilo amesema.

Lawrence Kanyuka amechapisha ujumbe kwenye ukurasa wake wa mtandao waa X, akitangaza kuwa AFC imejitolea kwa suluhisho la mazungumzo ya mgogoro.

Amesema hatua hiyo inalenga kuwezesha utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa hivi karibuni katika mkutano wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na mkutano wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika. Kanyuka amesema:îMaazimio haya yanatoa wito wa kusitisha mapigano kati ya pande husika na mazungumzo ya kisiasa kati ya Serikali ya Kongo na AFC/ M23. Tunatumaini kuwa serikali, wakati huu, itaheshimu na kutekeleza kikamilifu maazimio haya.î

Katika taarifa tofauti, muungano wa waasi uliishutumu serikali ya DRC na wanamgambo washirika wao kwa kuendelea kufanya mashambulizi ya ardhini na angani dhidi ya raia katika maeneo kadhaa, hasa Uvira na Minembwe katika jimbo la South Kivu.

Hayo yanajiri wakati ambao Tanzania jana Jumatatu, ilikuwa ni mwenyeji wa mkutano wa kikanda, kufuatilia matukio ya nyanjani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuchukua hatua zinazohitajika za kukabiliana na mgogoro huo.

Mkutano huo unahudhuriwa na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Katika mapigano ya hivi karibuni, waasi wa M23 wameteka miji miwili mikubwa ya DRC ambayo ni Goma na Bukavu katika eneo lenye utajiri wa madini la mashariki mwa nchi hiyo.






# YANGA YAMPA AZIZI KI JUKUMU ZITO JUMAMOSI

>> Inatoka uk. 16

lililokusanya idadi kubwa ya mastaa Jijini Dar, mashabiki wa timu hiyo na hata wapinzani wao walianzisha minong'ono wakidai huenda kiwango cha mwamba huyo uwanjani kinaweza kupungua kutokana na matumizi ya ndoa yaliyomkabili kwa zaidi ya wiki nzima.

Lakini tofauti na matazamio hayo mwamba huyo akawa ndiyo kama amezidisha moto, kwani alikuwa akipachika mabao na kutoa asisti katika mechi mbalimbali zilizofuata na kuisaidia timu yeke kudumu kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha Pointi 58.

Uimara huo ndiyo uliomfanya awe tegemeo la kikosi hicho katika mechi hiyo muhimu ijayo Jumamosi hii itakayowakutanisha dhidi ya Simba, ambapo furaha ya mashabiki wa Wanajangwano hao ni kumuona Aziz Ki akianza kukitumikia kikosi cha kwanza.

Mechi hiyo imeanza kuteka simulizi kwa asilimia kubwa katika miji mbalimbali na hasa vijiwe vya mijini vinavyokutanisha mashabiki wa Simba na Yanga.

# KARIA ARIDHIA ULIPAJI KODI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania-TFF, Bw. Wallace Karia, amekubali mapendekezo ya Serikali na kuahidi kuwa suala la ulipaji kodi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Aidha ameahidi kuwa watalichukulia kwa uzito suala la Kodi katika michezo yote ya mpira wa miguu inayosimamia na Taasisi hiyo.

Kauli hiyo imetolewa katika kikao cha majadiliano kati yake na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Na (Mb) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi. Kikao hicho pamoja na masuala ya kodi walijadili maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya michezo hususan mpira wa miguu nchini. Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, Serikali imeipongeza TFF na Bodi yake ya Ligi, kwa kusimamia kwa weledi masuala ya maendeleo ya soka na kuliletea Taifa heshima kubwa barani Afrika kiasi cha kupewa jukumu la kuandaa mashindano ya CHAN na AFCON.

Pia serikali ilikubaliana na namna tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo inavyoweza kutumika kuhamasisha uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari, kupitia kampeni ya kudai na kutoa risiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Majadiliano hayo yaliwashirikisha viongozi wa juu wa Wizara ya Fedha, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Bw.Yusuph Mwenda, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania- TFF, Bw. Wallace Karia, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Bw.. Almas Kasongo, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zinazosimamia michezo nchini.





# P-SQUARE

## 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-5

LOGOS, NIGERIA

NI lazima ieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.


Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.

Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.



# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'



UK. 15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA MICHEZO

JUMANNE Machi 04, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

# Yanga yampa Azizi Ki jukumu zito Jumamosi




NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Yanga kama ilivyo kwa wenzao wa Simba wanachotamani ni kuona timu yao inashinda tu dhidi ya Simba na siyo vingine, lakini kazi hiyo licha ya kufanywa na wachezaji mbalimbali ndani ya kikosi cha Wananchi hao, lakini macho mengi zaidi yameelekezwa kwa 'Bwana harusi' Aziz Ki.

Staa huyo ndani ya kikosi cha Yanga hivi karibuni alidumu midomoni mwa mashabiki na wapenda burudani kwa ujumla, pale alipofunga ndoa ya kifahari na msanii maarufu Tanzania Hamisa Mobeto.

Muda mfupi baada ya kufanyika tukio hilo

Inaendelea Uk.14

# ELIE MPANZU ABEBA MATUNAINI YA SIMBA

NA MWANDISHI WETU

SIKU zinazidi kukimbia kuelelekea mchezo wa soka wa kihistoria nchini, utakaozikutanisha timu kongwe Yanga na Simba zitakazogombea Pointi tatu kila moja, ukiwa ni mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya NBC.

Klabu hizo kongwe Yanga ilianzishwa mwaka 1935 kisha Simba ikafuata mwaka mmoja baadaye 1936 huwa hazina mechi ya kirafiki, kila zinapokutana ni vita kuu kuanzia mashabiki mpaka wachezaji wenyewe ndani ya uwanja.

Safari hii timu hizo zinakutana zikiwa katika wakati muhimu kwa kila moja ikitaka kushinda ili ijiweke vizuri katika msimamo wa ligi.

Ifahamike kwamba Yanga wanautaka zaidi mchezo huo kwa vile ushindi wa Jumamosi hiyo ya Machi 8, utaihakikishia nafasi ya kutetea ubingwa wake iliyoutwaa kwa misimu mitatu sasa.

Endapo itapoteza mchezo huo huenda kauli ya watani wao wa jadi Simba itakuwa inaanza kutimia, kwani mwanzoni tu mwa michuano hii ilitangaza vita rasmi ya

Inaendelea Uk.14




# MAN U, MAN CITY WAINGIA VITANI



LONDON, UINGEREZA

WABABE wa Soka la Jijini la London Manchester United wamejikutya wakitamani sehemu inayofikiriwa na watani zao wa jadi Manchester City wakimwania winga machachari Raia wa Ureno Francisco Trincao.

Klabu hizo mbili kila moja inahaha kupata saini yake lakini bado kuna

Inaendelea Uk.14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM